JINA …… KIDATO CHA KIDATO CHA TANO MWAKA 2018/19

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO

SHULE YA SEKONDARI EMBARWAY,

S. L. P. 41 NGORONGORO

S.L.P 41

Tarehe 18/05/2018

KUMB NA. ESS/STD/JNG V./2018/01

Namba za simu

Shule ya Sekondari Embarway

Mkuu wa Shule 0755990912

Makamu Mkuu wa Shule 0766086309

Matron 0766915019

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI EMBARWAY HALMASHAURI YA NGORONGORO MKOA ARUSHA MWAKA 2018/19.

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2018 tahasusi ya HKL, HGK, HGE na CBG shule ya Sekondari Embarway ipo umbali wa kilometa 283 kaskazini/ mwa mji wa Loliondo usafiri wa basi kutoka mjini Karatu unapatikana katika kituo cha mabasi Karatu Stendi nauli ni shilingi 7000/=

Muhula wa masomo unaanza tarehe 02/07/2018 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 02/07/2018 mwisho wa kuripoti ni tarehe 20/07/2018.

JINA …… KIDATO CHA KIDATO CHA TANO MWAKA 2018/19.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE ZA SHULE

a) Sare ya shule hii ni sketi 2 Estem nzito mukidoma (kijivu yenye rangi ya kijani kwa mbali kama ilivyo kwenye sampuli)

b) Rangi ya hijab (kijuba) ni (nyeupe)kama inavyoonekana kwenye sampuli

c) Sare ya michezo kwa shule ni raba nyeupe jozi 01 stoking nyeupe 2 bukta nyeupe pea 01 naTtracksut 01(dark blue)

d) Viatu vya shule ni vyeusi (simple) visiwe na urembo wowote vyenye visigino vifupi

e) Soksi jozi mbili nyeupe za shule

f) Sweta 02 rangi mukidoma kama ilivyo kwenye sampuli

g) Nguo za kushindia (shamba dress) 02 rangi ya damu ya mzee,T- shirt 02 za kushindia zenye nembo ya shule

h) Tai 2 rangi ya darkblue yenye mistrari meupe na T- shirt 02 za darasani zenye nembo ya shule

i) Shati mbili nyeupe mikono mirefu.

2.2 ADA NA MICHANGO YA SHULE

Ada ya shule kwa mwaka ni shilling 70,000/= kwa mwanafunzi wa bweni unaweza kulipa kiasi cha shilling 35,000/= kwa nusu muhula au kulipa ada yote kwa mara moja kwa muhula mzima. Michango mingine ni kama ifuatavyo:-

i. Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani

ii. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha

iii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma

iv. Shilingi 30,000 kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine

v. Shilingi 2,000/= nembo ya shule

vi. Tsh 5000 tahadhari (hairudishwi)

vii. Shilingi 20,000/= mitihani ya kujipima mock

viii. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza Tsh 5,000/= na bima ya afya Tsh 5,000/= (Mwanafunzi anashauriwa kujiunga na Mfuko wa Bima ya afya CHF kikaya. CHF card italipia gharama za vipimo na dawa tu).

NB: Huduma ya kwanza itatolewa shuleni. Endapo mwanafunzi atalazwa au atahitaji matibabu zaidi nje ya shule kulingana na ugonjwa aliyonao basi mzazi atagharamikia matibabu hayo, hivyo shule haitahusika tena.

Angalizo: Jumla ya ada na michango kwa wanafunzi wa bweni ni **shilingi 178,000/= kwa mwaka. Usilipe zaidi**

Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule Na40901000004 ni katika Benki ya NMB jina la A/C ni EMBARWAY SECONDARY SCHOOL (tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip)

b) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni

i. Ream ya karatasi 1 A4 kwa ajili ya shule na ream 01 kwa ajili ya matumizi yake kwa mwaka.

ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatanishwa) ingawa shule ina vitabu vya kutosha

iii. Scientific calculator kwa wanafunzi wa sayansi

iv. Godoro kwa wanafunzi wa bweni 01 (size) 3"x 6ft x 3ft (tanform/Dodoma)

v. Mashuka pair 02 pinki ,blanketi 01, Taulo, chandarua 01, nguo za ndani vitano kila mmoja

vi. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe vyote vya aluminum (bati)

vii. Ndoo moja ndogo yenye mifuniko

viii. Ruber squeezer 02 ,Hardbroom 01 (vifaa hivyo atatumia yeye mwenyewe)

MUHIMU: Kumbuka kuja na result slip na cheti cha Kuzaliwa

MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI AONDOLEWE SHULENI

i. Wizi

ii. Kutohudhuria masomo kwa ziadi ya siku 90 bila taarifa/utoro

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyto yule

vi. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya

vii. Uvutaji wa sigara

viii. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa

ix. Kupata ujauzito au kutoa mimba

x. Kushiriki matendo ya uhalifu , siasa na matendo yoyote yale yanayavunja sheria za nchi

xi. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana

xii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni

xiii. Kumilliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule

xiv. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi

xv. Kufanya jaribio la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.

xvi. Kudharau Bendera ya Taifa

VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU ZA KUJAZA

FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA KIDATO CHA TANO 2018/19

Fomu hii ijazwe na mzazi/mlezi pamoja na mwanafunzi aliyechaguliwa kuingia kidato cha tano kisha iletwe shuleni siku ya kuripoti (ithibitishwe na mwenyekiti/Afisa mtendaji wa kijiji wa eneo unaloishi)

Mimi …… kwa hiari yangu ninakubali/sikubali nafasi niliyopewa ya kuingia kidato cha tano 2018/2019 katika shule ya Sekondari Embarway. Nitakuwa tayari kuzifuata sheria za shule kama ilivyoandikwa kwenye ukurasa wa 3 wakati na nitastahili aidha kuchukuliwa hatua za kinidhamu au kusimamishwa masomo. Endapo nitatenda makosa yaliyoainishwa, kuwa yanaweza kunifukuzisha shule mara moja kabla sijaleta athari kubwa kwa shule kinidhamu na kitaaluma.

Tarehe …….. ……

Sahihi ya mwanafunzi

Mimi …… mzazi/mlezi wa …….

Nakubali/ sikubali nafasi aliyopewa mtoto wangu na kwamba muda wote awapo shuleni analazimika kufuata sheria za shule kama ilivyoainishwa hapo juu na kuwa mtiifu kwa walimu ambao ndio walezi wake.

 Nitahakikisha kuwa michango yote ya shule nitalipa kwa wakti na mahitaji ya mtoto wangu nitampatia kila wakati bila usumbufu. Endapo sitatekeleza wajibu wangu mwanangu arudishwe nyumbani na nichukuliwe hatua za kisheria mara moja kwa kushindwa kutekeleza wajibu wa mwanangu kama mzazi au mlezi

 Pia nitahakikisha kuwa mtoto wangu atakuwa shuleni kwa kipindi chote cha masomo, na endapo atashindwa kuja shuleni kwa sababu zozote nitatoa taarifa kwa mwalimu mapema nimeelewa kuwa akiacha shule kwa siku 90 kwa siku mfululizo kama sheria ya wizara husika inavyosema atakuwa amejifukuzisha shule.

 Nitahudhuria viakao vyote vya wazazi shuleni na kufuatilia ukaribu wa maendeleo ya mwanangu kinidhamu na kitaaluma.

……. Tarehe ……

Sahihi ya mzazi/mlezi

Mimi …….. ninathibitisha kuwa ndugu …….. ni mzazi/ mlezi wa mtoto huyu aliyechaguliwa kuingia kidato cha 5 Embarway sekondari 2018.

…….. tarehe ……

Sahihi ya mwenyekiti wa mtaa/kijiji

Muhimu: Fomu zote kuanzia ukrasa wa 3 hadi ukurasa wa 7 lazima kurudishwa ofisini zikiwa zimejazwa vizuri na kutiwa saini na wahusika wote kwani ndiyo fomu zitakazofungua jalada la mwanafunzi. 5

JINA …….KIDATO CHA TANO MWAKA 2018/19

Mimi …….. nimesoma sheria za shule na taratibu zote naahidi kuzitekeleza kwa uaminifu mkubwa na kufuata ushauri wa walimu.

Nitahudhuria masomo yote kila siku; na kufanya mazoezi, majaribio yote na mitihani yote kikamilifu. Sitashiriki katika hila zozote za wizi au udanganyifu wa mitihani, nitashiriki katika klabu za kimasomo na michezo mbalimbali shuleni na wala sitaacha shule kamwe bila taarifa.

Nitahudhuria maandalio (preparation) yote ya mchana na usiku ili kujisomea na si kwingineko kokote. Nifukuzwe shule mara moja endapo nitaonekana nazurura mitaani, porini (wakati wowote) au bwenini wakati wa vipindi au kujisomea siku za masomo, au siku za jumamosi na jumapili (week-ends).

Ninaahidi kusoma kwa bidii na kuwatumia walimu wangu vizuri kitaaluma na nitatii mashauri yote yanayotolewa na wazazi/walezi na walimu wangu siku zote.

Michezo ninayoshiriki vizuri

1. ……

2. ……

3. ……

Naweza kushiriki vema katika fani za ndani.

1. Kwaya ( )
2. Ngoma ( )
3. Maigizo ( )
4. Ngonjera ( )
5. Muziki ( )

Weka (√) kubainisha unavyoweza kushiriki.

Nitashiriki kikamilifu katika kazi zote za mikono, natambua kuwa migomo na vurugu ni haramu hivyo sitashiriki wala kushawishi wengine kujihusisha.

Nitawasilisha matokeo ya mitihani na majaribio pamoja na barua nitakazopewa shuleni kwa mzazi/mlezi wangu.

JINA LA MWANAFUNZI……

SAHIHI ……

TAREHE ……

HABARI ZA MWANAFUNZI

1. Jina kamili …… ..(majina matatu)
2. Tarehe ya kuzaliwa ……..(kama ilivyo kwenye cheti)
3. Dini …… dhehebu ……..
4. Mahali na wilaya alipozaliwa …….
5. Shule ya sekondari alikohitimu kidato cha nne……..

6. Mambo anayopendelea kufanya nje ya masomo

a) ……b) ……. c) …….

HABARI ZA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili la baba……..(majina matatu)
2. Kazi yake ……dini ……..
3. Jina kamili la mama ……(majina matatu)
4. Kazi yake …….. dini ……
5. Anwani ya mzazi onyesha ni baba au mama …….baba/mama

Simu ……..(baba)…….(mama)

6. Nyumbani (mahali anapoishi baba/mama wa mtoto , Wilaya …… kijiji……kata……
7. Jina la M/kiti wa mtaa……..
8. Jina kamili la mlezi…… Iwapo mtoto haishi na wazazi wake
9. Anwani kamili ya mlezi ……. Simu……..
10. Dhehebu atokalo mzazi mtoto wake alelewe……..
11. Anuani kamili ya nyumbani ambako mtoto atakwenda siku za likizo

……

……

…….

12. Ndugu wa mwanafunzi wakatakaokuja kumtembelea mwanao

JINA SAHIHI

i. ..... ……

ii. ……. ……

iii. ..... ……

iv. ……. ……

v. …… ……

Mimi ……baba/mama/mlezi wa ……nathibitisha kuwa taarifa hizo hapo juu ni sahihi na ninaahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba mwanangu anakuwa na tabia nzuri, mwenye bidii ya masomo na asiyezurura mitaani nyakati za masomo na hata siku za weekend.

PRESIDENT OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
NGORONGORO DISTRICT EMBARWAY SECONDARY SCHOOL
MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by **Medical officer only**

Name of student
……..……..Age……..……

1. HIV test ……
2. Blood count (White & red)……
3. Urine examination ……
4. UTP…….(For female)
5. Stool examination ……
6. Syphilis test ……
7. TB test ……
8. Ear test ……
9. Eye test ……
10. Abdomen ……
11. Spleen ……
12. Additional information or any other physical, mental hereditary or infections diseases
    ……..
    (please state nature of treatment)

Medical certificate

I certify that the above mentioned student has been examined and found him/her to be fit/unfit to pursue further education.(delete whichever not needed)

Name …… signature ……
Designation …… station ……
Date ……

Official stamp

NB fomu hii lazima ijazwe na Daktari katika Hospitali inayotambulika na serikali

NB: Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatelekeza kikamilifu

S/NO	**TITLE**	**AUTHOR**
	KISWAHILI 1 &2	
1.	FASIHI YA KISWAHILI	MULOKOZI M.M 1996
2.	UFUNDISHAJI WA FASIHI NADHARIA NA MBINU	KIMANI W NA C. ROCHA 1999
3.	MISINGI YA UKALIMANI	F. S. WANJALA
4.	DAFINA YA LUGHA	RIROK SMATIRODE
	ENGLISH 1&2	
1.	ADVANCED ENGLISH PAPER TWO FOR FORM FIVE AND SIX SYNOPTIC LITERATURE	SIEP – TANZANIA WITH JULIANA WAMENDA
2.	ENCOUNTERS FROM AFRICA AN ANTHOLOGY OF SHORT STORIES	MAC MILLAN – KENYE
3.	A TEXT BOOK OF TRANSLATION	NEW MARK, P
4.	THE LINGUISTIC SCIENCE AND LANGUAGE TEACHING	HALLIDAY
	GENERAL STUDIES	
1.	UNDERSTANDING ADVANCED LEVEL GENERAL STUDIES	BIGIRWAMUNGU AND SOSPETER M. DEOGRATIAS
	HISTORY 1&2	
1.	HOW EUROPE UNDERDEVELOPED AFRICA (182)	WALTER RODNEY
2.	HISTORY OF EAST AFRICA BK I	
3.	MODERN WORLD HISTORY 182	CHANCEL M. WEIGHT J.
4.	ADVANCED APPROACH TO AFRICAN HISTORY 182	MUSHEGA A.M
5.	HISTORY OF MODERN EUROPE	PEACOCK H.
	GEOGRAPHY 1&2	
1.	ORDINARY SURVEY MAP WORK	B.D.R WORTHINGTON AND ROBERT GRANT
2.	MAP READING FOR EAST AFRICA	D.N MC MASTER
3.	SIMPLIFIED GEOGRAPHY	JOSEPH MILIAN
4.	A PRACTICAL GUIDE TO STATISTICAL MAPS AND DIAGRAMS	TRURAN H.E
5.	SOIL AND CLIMATOLOGY (PLANT GEOGRAPHY)	ZISIT. KAMILI
	BIOLOGY 1&2	
1.	ADVANCED LEVEL CLASSIFICATION	JOSEPHAT
2.	ADVANCED LEVEL BIOLOGY , REPRODUCTION AND GENETICS	MWL. MANDIA
3.	ADVANCED LEVEL BIOLOGY, TRANSPORT ECOLOGY GROWTH AND EVOLUTION	MWL. MANDIA
4.	ADVANCED LEVEL BIOLOGY, CYTOLOGY NUTRITION AND BIOCHEMISTRY	MWL. MANDIA
5.	FUNDAMENTAL CONTEXT OF A- LEVEL BIOLOGY VOLUME 1	BOAZ .H AND OTTENYO
6.	ADVANCED LEVEL BIOLOGY CO – ORDINATION RESPIRATION, GASEOUS EXCHANGE, EXCRETION, OSMOREGULATION AND HOMEOSTASIS	JOSEPHAT AND MANDIA
7.	BIOLOGY FOR CLASS XII P.S	P.S VERMA AND B.P PANDEY
	CHEMISTRY 1&2	
1.	PHYSICAL CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL	NFAIZA
2.	ORGANIC CHEMISTRY PRACTICAL 1 AND II	JOSEPHAT
3.	SOIL CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL	MANDIA
4.	INORGANIC CHEMISTRY	MANDIA
5.	GENERAL CHEMISTRY	
	BASIC APPLIED MATHEMATICS	
1.	BASIC APPLIED MATHEMATICS	TANZANIA INSTITULE OF EDUCATION
2.	BASIC APPLIED MATHEMATICS , PROBLEMS AND SOLUTIONS	YAHYA KAWIA

MFANO WA SARE ZA SHULE (MASHONO NA RANGI)

SARE ZA DARASANI

SARE BAADA YA MASOMO

NB: **KWA MZAZI ASIYEWEZA KUELEWA VIZURI SARE HIZI NI VEMA MWANAFUNZI ARIPOTI KWANZA NDIPO ASHONEWE SARE BAADAYE,**

EMBARWAY SECONDARY SCHOOL ADMNISTRATION BLOCK

MOTTO WETU: *ELIMU NI UKOMBOZI*

KARIBU SANA EMBARWAY

TOONDE L. S. SULLE

MKUU WA SHULE